**HOTUBA YA MSEMAJI MKUU WA KAMBI RASMI YA UPINZANI BUNGENI MHESHIMIWA HAMIDU HASSAN BOBALI (MB) WIZARA YA MAJI NA UMWAGILIAJI KUHUSU MAPITIO YA UTEKELEZAJI KWA MWAKA WA FEDHA 2016/2017 NA MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA WIZARA KWA MWAKA WA FEDHA 2017/18**

*(Yanatolewa chini ya Kanuni za Bunge, Kanuni ya 99(9), toleo la mwaka 2016)*

## 1.0 UTANGULIZI

**Mheshimiwa Spika,** kwanza kabisa nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu, kwa kunijalia afya njema inayoniwezesha kusimama mbele ya Bunge lako Tukufu kuwasilisha maoni na mapendekezo ya Kambi Rasmi ya Upinzani kwa Wizara hii.

**Mheshimiwa Spika**, kipekee kabisa naomba nichukue fursa hii adhimu kumpongeza Mhe. Peter Lijualikali (Mb), Naibu Msemaji Mkuu wa Wizara hii kwa kufanikiwa kuandika historia adhimu ya kuhukumiwa kufungwa jela wakati akiwa anapambana kuwatetea wapiga kura wake wa Jimbo la Kilombero, pia akiwa anatetea haki yake ya kupiga kura katika halmashauri ambayo yeye ni Mbunge wa kuchaguliwa.

**Mheshimiwa Spika,** nampongeza Mhe. Lijualikali sio tu kwa kuwa ameshinda rufaa yake na hivyo kuwa huru kuwatumikia wapigakura wake, bali pia kitendo chake cha kufungwa huku akiwa mbunge wakati hakuwa na makosa. Hii imeionesha Dunia kuwa wanaofungwa katika nchi yetu sio kuwa wote wanakuwa na hatia.

Jina lake litakuwa rejea mbalimbali katika vitabu na majarida mbalimbali Duniani kote. Lijualikali umekuwa mwakilishi wa wanaofungwa bila hatia na shujaa wa vijana wote wa Tanzania.

**Mheshimiwa Spika,** mwisho lakini kwa umuhimu mkubwa ni shukrani kwa wanachama wa CUF na wananchi wa Jimbo la Mchinga kwa kuendelea kunipa ushirikiano mkubwa katika utendaji kazi wangu wa shughuli za kibunge na kichama, bila kusahau kwa umoja wetu ndiyo silaha ya kuhakikisha bwana Yule anaondoka kwa aibu.

## 2.0 MUUNDO NA MFUMO WA KISEKTA

**Mheshimiwa Spika,** ninapowasilisha hotuba hii ya Wizara Kivuli ya Maji na Umwagiliaji kutoka katika Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni, ninaomba niazime tamko la kauli mbiu za kitaifa na kimataifa kuhusu umuhimu wa maji. Kauli mbiu hizi ni pamoja na tamko la Kimataifa kwamba ***"Maji ni Haki ya Kibinaadamu, Maji ni Uhai, Maji ni Uchumi; Maji ni Msingi wa Amani na Maji ni Siasa".***

***Mheshimiwa Spika,*** *kabla ya kuingia kwa undani katika utoaji wa maoni na uchambuzi wa wizara, Kambi Rasmi inamtaka Mheshimiwa Waziri awaeleze watanzania kwa kujibu swali hili, maji ni huduma au biashara?*

**Mheshimiwa Spika,** umuhimu wa maji kwa ajili ya uhai wa watu, wanyama, mimea na mazingira kwa ujumla ni jambo lisilopingika. Bila ya maji, viumbe vyote

vitapotea, mazingira yatakuwa mfu, na maendeleo ya kiuchumi na ya kijamii yatadumaa.

Kutokana na umuhimu wa maji, Baraza Kuu la Umoja wa Mataifa katika kikao chake cha tarehe 21 Desemba 2016 limeridhia kwa kauli moja miaka kumi ya utekelezaji wa **Azimio jipya la Maji kwa Maendeleo Endelevu (Interational Decade (2018-2028) for Action-Water for Sustainable Development).**

**Mheshimiwa Spika,** Dira ya Maendeleo ya Taifa (Tanzania Development Vision 2025) imeweka malengo ya maendeleo ya kiuchumi, kisiasa na ustawi jamii ikiwa ni pamoja na malengo yanayogusa moja kwa moja Wizara na Sekta ya Maji na Umwagiliaji. Baadhi ya malengo muhimu katika muktadha huu ni kama ifuatavyo:

i. Tanzania kuwa nchi ya uchumi wa kati, ambapo wananchi wake wanafurahia amani na umoja wa kitaifa

ii. Upatikanaji wa maji safi na salama kwa wakazi wote. Ambapo kwa wakazi wa mijini watapata maji kwa asilimia 100 na kwa wakazi wa vijijini watapata maji safi na salama kwa agalau asilimia 90 ifikapo 2025.

iii. Kuhakikisha kwamba raslimali za maji ni endelevu ili kukidhi mahitaji ya kiuchumi na kijamii.

**Mheshimiwa Spika, i**li kufikia malengo ya Dira ya Taifa ya Maendeleo (2025), Serikali ya Jamhuri ya Muungano

wa Tanzania kupitia Wizara ya Maji na Umwagiliaji inatekeleza programu kuu zifuatazo:

i. Programu ya Maendeleo ya Sekta ya Maji (Water Sector Development Programme-WSDP)

ii. Programu ya Maendeleo ya Sekta ya Kilimo (Sekta ya Umwagiliaji inayosimamiwa na Tume ya Taifa ya Umwagiliaji).

**Mheshimiwa Spika,** Programu ya Maendeleo ya Sekta ya Maji (Water Sector Development Programme-WSDP) ni mradi wa muda mrefu wa utekelezaji wa miaka ishirini. Utekelezaji wake ulianza mwaka 2006 na utafikia ukomo wa utekelezaji mwaka 2025 ambapo inategemewa kuwa viwango vya upatikanaji wa maji safi na salama na usalama wa maji kwa ujumla vitakuwa vimefikiwa.

**Mheshimiwa Spika,** ili kuwezesha utekelezaji wa programu kubwa ya kiwango cha WSDP ya Tanzania, programmu imegawanywa katika awamu kuu nne za utekelezaji, ambapo kwa sasa awamu ya kwanza iliyochukua takriban miaka minane imemalizika, na sasa awamu ya pili inatekelezwa Muundo na mfumo wa utekelezaji umegawanya programu hii katika sehemu kuu zifuatazo:

i. Usimamizi wa Raslimali za Maji.
ii. Huduma ya Maji na Usafi wa Mazingira Vijijini
iii. Huduma ya Maji Usafi wa Mazingira na Uondoshaji wa Maji Taka Mijini

iv. Usafi wa Mazingira na Usafi Mashuleni (National Sanitation Campaign and School WASH)
v. Mfumo wa Uwezeshaji wa Utekelezaji wa Programmu (Programme Delivery Support)

**Mheshimiwa Spika, u**tekelezaji wa programu hii unafanyika kwa kuzingatia sera kuu za maendeleo ya taifa, Sera za kisekta kama vile Sera ya Maji ya mwaka 2002; Sera ya Ugatuaji wa Madaraka (Decentralization by Develution); Mikakati ya Kupunguza Umaskini nchini, na Mpango wa Pili wa Maendeleo ya Taifa wa Miaka Mitano. Majukumu na wajibu wa wadau wa Sekta ya Maji hususan wale wanaohusika na utekelezaji wa programmu hii wanatajwa kuwa katika ngazi ya Taifa ni pamoja na Wizara ya Maji yenyewe, Wizara za Afya, Elimu na Ofisi ya Raisi Tawala Za Mikoa na Serikali za Mitaa, na washirika wa kitaifa na kimataifa ikiwa ni pamoja na taasisi za kifedha za Kitaifa na kimataifa.

**Mheshimiwa Spika,** Sera ya Taifa ya Maji ya mwaka 2002, imeweka bayana umuhimu wa Sekta Binafsi (private sector) katika utoaji wa huduma ya maji kwa wananchi wa Tanzania. Hivyo basi sekta binafsi ni mmoja kati ya wadau wakuu wanaotoa huduma kama vile za utafiti; uchimbaji na ujenzi wa miundombinu, fedha, utawala, mafunzo, na upatikanaji wa vipuri.

**Mheshimiwa Spika,** Katika ngazi za Kanda, Mikoa, Wilaya na Vijiji programu inatekelezwa kupitia Bodi za Mabonde ya Maji (Basin Water Boards); Mamlka za Maji Mijini na kipekee kwa sababu ya unyeti wake Mamlaka ya Maji ya jiji la Dar-es-Salaam; Mamlaka za

Maji katika makao makuu ya Wilaya na Miji Midogo; na Halmashauri za Wilaya kupitia idara ya Mhandisi wa Maji. Katika ngazi ya kijiji, wadau wakuu wa usambazaji wa maji safi na salama kwa wananchi ni pamoja na Serikali za Vijiji, na Vyombo vya Watumiaji wa Maji (Community Owned Water Supply Organisations) ambavyo ni taasisi rasmi za kijamii zenye mamlaka ya kisheria za kuendesha vituo vya usambazaji wa maji vijijini.

**Mheshimiwa Spika, n**imeona ni vyema kutumia fursa hii kuelezea kwa kina muundo na mfumo wa utoaji wa huduma ya Maji safi na Salama kwa Umma wa Watanzania kupitia  Bunge lako Tukufu kwa sababu mpaka hivi sasa bado watanzania wengi wa mijini na vijini bado hawana ufahamu wa mabadiliko yaliyofanywa katika Utekelezaji wa Sera ya Taifa ya Maji  ya Mwaka 2002 (National Water Policy – NAWAPO 2002); pamoja na utekelezaji wake kupitia Programmu ya Taifa ya Maendeleo ya Maji.

**Mheshimiwa Spika,** Ikumbukwe ya kwamba utekelezaji wa WSDP unafanywa kupitia sheria kuu mbili za maji pamoja na kanuni zake na miongozo mbali mbali yaani Sheria ya Maji na Usafi wa Mazingira ya Mwaka 2009; na Sheria ya Raslimali za Maji ya Mwaka huo huo.

**Mheshimiwa Spika,** Pamoja na kuwa na mfumo maalum wa kitaasisi kwenye sekta kwa ajili ya uwezeshaji na uendeshaji wa programmu, ufahamu wa watanzania kuhusu mabadiliko ya kisera, kisheria na kitaasisi ndani ya sekta ya bado ni mdogo, jambo ambalo linadhoofisha kanuni ya ushirikishaji, utawala

bora na uwazi katika uboreshaji na utoaji wa huduma za maji na usafi wa mazingira mijini na vijijini.

**Mheshimiwa Spika,** Taarifa mbali mbali za utafiti kuhusu ushiriki wa jamii na wadau mbali mbali wa Sekta ya Maji katika utekelezaji wa WSDP unaonesha kuwa wadau wengi hawana ufahamu wa miundo na mifumo ya programmu jambo linalochangia utekelezaji hafifu wa mradi.

**Mheshimiwa Spika,** Nitatoa mifano michache kuhusu jambo hili. Hali halisi ilivyo huko vijijini inaonesha kuwa bado vijiji vingi nchini vinatekeleza shughuli za usambazaji wa maji kupitia "kamati za maji' na siyo Vyombo vya Watumiaji wa Maji (COWSOs) kama inavyotakiwa kisheria.

**Mheshimiwa Spika,** Kambi Rasmi ya Upinzani kwa kutambua umuhimu wa maji kwa wananchi wa Tanzania imefuatilia kwa kina utekelezaji wa WSDP awamu ya Kwanza na WSDP awamu ya II.

**Mheshimiwa Spika**, Kati ya changamoto zilizooneshwa katika utekelezajiwa wa awamu ya kwanza ya Programu ni programu awamu ya kwanza na vile vile katika utekelezaji wa mpango na bajeti 2016/17 suala la uundaji wa Vyombo vya Watumiaji wa Maji limebaki kuwa ni changamoto kubwa na linalochangia kwa kuharibika kwa miundobinu ya maji kwa kasi kubwa, kwa kukosekana ka usimamizi wa karibu wa miundo mbinu ya maji karibu na vituo vya kuchotea maji.

**Mheshimiwa Spika,** kulingana na taarifa za hivi karibuni, Tanzania inapiga hatua moja mbele katika kutoa huduma ya maji lakini inarudi hatua mbili nyuma katika

utoaji wa huduma hiyo kutokana na kuharibika kwa miundombinu na upotevu mkubwa wa maji safi na salama yanayozalishwa kwa fedha nyingi

**Mheshimiwa Spika,** Wataalamu na Wadau wa Sekta ya Maji wanajuliza maswali mengi na hivi karibuni kupitia ukurasa wa Mtandao wa taasis bobezi ya Maji kumekuwa na swali la msingi kama ifuatavyo na ninanukuu kwa kiingereza kama ilivyo:

> *"Despite massive investments in rural water supply in Tanzania, the number of people with access to improved water sources has not increased. This begs the question, what could be the reason for this stagnation?"*
>
> (http://www.ircwash.org/blog/rural-water-supply-access-tanzania-why-has-it-stagnated)

**Mheshimiwa Spika**, taarifa iliyotolewa na wataalmu hao ni kwama kwa kila mtanzania mmoja anayepata huduma ya maji safi na salama, wapo wawili wanaokosa huduma hiyo, hususan vijijini. Taarifa hiyo ikinukuu taarifa za mfumo wa ufuatiliaji na tathmini wa kimataifa juu ya maendeleo ya maji na usafi wa mazingira unaonesha kuwa upatikanaji na usambazaji wa maji ni mdogo sana kulinganisha na takwimu zinazotolewa na Wizara.

**Mheshimiwa Spika,** Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaitaka wizara ya Maji ituambie je, ni kwa kiasi gani Wizara ya Maji imewianisha mfumo wake wa tathmini na ule wa Ufuatiliaji na Tathmini wa kimataifa (joint Monitoring programme au JMP?). Je tuamini kipi kati ya

takwimu za Kitaifa na zile za JMP? Na sababu ya kuamini kimojawapo ni nini?

**Mheshimiwa Spika,** Kambi ya Upinzani Bungeni inaamini kuwa Mkakati wa Maendeleo Endelevu wa Sekata ya Maji (Sustainability Strategy) ulioandaliwa na kuasisiwa na Sekta hii kwa fedha nyingi za walipa kodi wa Kitanzania na wale wa nchi za nje haujapewa kipaumbele stahiki hususan katika suala la kuanzisha na kuwezesha Vyombo vya Usimamizi wa Maji. Kwa sababu hiyo fedha nyingi zinazowekezwa kwenye sekta hii hupotea bure,

**Mheshimiwa Spika,** Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inataka Serikali kuuelezea umma wa watanzania masuala yafuatayo:

i. Ni kiasi gani cha fedha kimetumika katika kuanzisha na kuimarisha vyombo vya watumiaji maji vijijini?
ii. Ni mkakati upi utatumika ili kuhakikisha kuwa vyombo ya watumiaji maji vinaundwa, vinaimarishwa na kusajiliwa rasmi ili kuwezesha utekelezaji wenye tija wa WSDP II vijijini?
iii. Kwa vile uwepo wa vyombo vya watumiaji maji ni sehemu ya Kigezo cha kupata Rusuku ya Maji inayojulikana kama “malipo kwa Matokeo” ni hatua zipi zimechukuliwa kufidia halmashauri amabzo zimekosa kupata ruzuku hiyo kwa kukosa sifa kutokana na kutokuwepo kwa vyombo vya watumiaji maji ?

## 3.0 UWEKEZAJI KATIKA SEKTA YA MAJI: BAJETI ZA SEKTA NA MWENENDO WAKE

**Mheshimiwa Spika,** Mpaka kufikia mwisho wa utekelezaji wa Awamu ya kwanza ya Programmu ya Maendeleo ya maji mnamo Juni 30 2016,fedha zilizowekezwa katika programu zilikuwa ni Dola za Kimarekani 1,713.5

Awamu ya pili ya utekelezaji wa Programu ya Maendeleo ya ya Maji. Programu hii ina sifa ya kuwa ni programu kubwa na pengine yenye kugharimu fedha nyingi kuliko programu nyingine za kitaifa barani Afrika *(MoWI: 2013 'WSDP Tanzania Evaluation of Phase 1)*.

**Mheshimiwa Spika,** Ninaomba pia kurejea bajeti za Sekta za maji na umwagiliaji kwa mwaka 2016/17, ili kuweka kumbukumbu vizuri. Katika Mwaka huo wa fedha, Wizara iliomba na kuidhinishiwa bajeti za Sekta za Maji na Umwagiliaji yaani kifungu namba 49 na kile cha namba 05 kama ifuatavyo:

### 3.1 HUDUMA ZA MAJI

**Mheshimiwa Spika**, Sekta ya maji (kifungu 49) mwaka wa fedha 2016/17 iliombewa bajeti ya Tshs 939,631,302,771 ambapo kati ya hizo, Tshs 915,193,937,771 ni kwa ajili ya maendeleo na Tshs 24,437,365,000 ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida yaani mishahara na matumizi mengineyo.

Bajeti hii ni takriban maradufu ya ile iliyoidhinishwa katika mwaka wa fedha uliopita yaani 2015/2016, ambapo kifungu namba 49 kiliidhinishiwa jumla ya Tshs 458,900,981,000 ambapo kati ya fedha hizo Tshs

427,257,904,000 zilikuwa ni kwa ajili ya shughuli za maendeleo na Tshs 31,643,077,000 zilikuwa ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida.

**Mheshimiwa Spika**, lakini hadi mwisho wa mwaka wa bajeti 2015/16 Wizara ilipokea fedha za maendeleo jumla ya shilingi 141,244,873,622 ambazo ni sawa na asilimia 33.06 ya fedha zilizokuwa zimeidhishwa na Bunge kwa ajili ya miradi ya maendeleo.

**Mheshimiwa Spika,** hadi kufikia mwezi Machi, 2017 fedha za maendeleo ambazo zilikuwa zimepokelewa na Wizara ni shilingi 181,209,812,609 sawa na asilimia 19.8 tu ya fedha zilizokuwa zimetengwa na Bunge.

**Mheshimiwa Spika**, takwimu hizo zinaonesha kuwa kuongezeka kwa takwimu za fedha haina maana kwamba fedha hizo zitatolewa kwa uwiano wa bajeti. Hivyo basi Kambi Rasmi ya Upinzani inaitaka Serikali kuacha kupanga bajeti inayotoa matumaini lakini haina uhalisia katika utekelezaji wa miradi.

**Mheshimiwa Spika,** Taarifa ya hali ya Sekta ya Maji ya Oktoba 2016 (Water Sector Status Report October 2016) imedhihirisha kuwa kufikia Juni 2016, fedha zilizopokelewa na Wizara kwa ajili ya utekelezeji wa programmu zilikuwa ni Tshs 510,377,900,552.22, ambapo kati ya hizo Tshs 235,521,926,883.85 zilitokana na malimbikizo ya fedha za nyuma kutoka kwa washirika wa maendeleo wanaotekeleza miradi maalum yaani ***earmarked projects***. Ukiondoa fedha hizo za malimbikizo, fedha zilizotolewa kwa ajili ya utekelezaji wa bajeti ya 2015/2016 zilikuwa ni aslimia 64, yaani Tshs

274,855,973,668.37 kati ya 510,377,900,552.22, zilizoidhinishwa.

**Mheshimiwa Spika,** Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni imeleta suala hili hapa ili kuonesha historia ya mkanganyiko katika mwenendo wa matumizi ya fedha za sekta ya Maji.

**Mheshimiwa Spika,** Ili kwenda mbele vizuri na mtiririko wa fedha za bajeti na matumizi yake kwa miaka inayofuatia, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inataka kupata maelezo ya ziada /kina kwa niaba ya watanzania watumiaji wa maji na walipa kodi; kuhusu hizo Tshs Tshs 235,521,926,883.85 kutoka kwenye ***earmarked projects.***

**Mheshimiwa Spika,** Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inarejea na kuelezea kwamba taarifa ya Hali ya Sekta ya Maji (WSSR Ocober 2016) haijafafanua ni katika miaka ipi malimbikizo hayo ya ***"earmarked project funding***" yamekuwa yakitolewa taarifa. Pili tunataka maelezo ya kina namna ambavyo fedha hizo zilivyoidhinishwa na baadaye kuingizwa kwa ujumla wake katika taarifa hiyo ya WSSR ya Okoba 2016.

**Mheshimiwa Spika,** Katibu Mkuu wa Wizara ya Fedha na Mlipaji Mkuu wa serikali Dr. Servacius Likwelile, mchana wa tarehe 11.10.2014 kwa niaba ya Serikali alitiliana saini makubaliano ya mkataba wa kuanzisha Mradi wa Maji katika Wilaya ya Same na Mwanga, na Mfuko wa maendeleo ya uchumi wa Kuwait akiwa Washington D.C

**Mheshimiwa Spika,** Mfuko huo wa Maendeleo ya Uchumi wa Kuwait ulitoa Dola za Kimarekani milioni 34.0 sawa na shilingi Bilioni 56.10 za Kitanzania kwa ajili ya kusaidia mradi wa maji katika Wilaya ya Same na Mwanga. Kambi Rasmi ya Upinzani inafahamu umuhimu wa mradi huo, kwa wananchi wa maeneo husika hadi maeneo ya Wilaya ya Korogwe ambao nao wangekuwa wanufaikaji wa mradi huo wa maji kutoka bwawa la Nyumba ya Mungu.

**Mheshimiwa Spika,** Kambi Rasmi ya Upinzani inataka kupata mrejesho wa mradi huo mkubwa wa maji umefikia wapi kwa kuangalia utekelezaji kwa mujibu wa thamani ya fedha?

### 3.1.1Raslimali za Maji na Usalama wa maji

**Mheshimiwa Spika,**

Hali halisi ya maendeleo ya maji nchini haiakisi Dira ya Maendeleo ya Taifa iliyotajwa hapo juu. Wizara ya Maji na Umwagiliaji inaelezea wazi kwamba Tanzania iliyokuwa na kiwango kikubwa cha uhakika wa maji inaelekea kuwa ni nchi yenye 'UHABA wa MAJI" ***(Water Stressed Country)*** iwapo hatua mathubuti na za haraka hazitachukuliwa.

**Mheshimiwa Spika,** Hotuba iliyosomwa Bungeni na Waziri wa Maji na Umwagiliaji Mei 2016, inaelezea wazi kuwa kwa sasa, raslimali za maji zinatosheleza kumpatia kila Mtanzania mita za ujazo 1,952 kwa

mwaka. Kiwango cha kimataifa za mahitaji ya mtu mmoja ni mita 1,700 kwa mwaka.

**Mheshimiwa Spika,** Hata hivyo kiashiria cha kustua katika hotuba hiyo ni kile kinachoonesha kuwa kama hatua za kiutawala, kitaalamu na kisiasa hazitachukuliwa, upatikanaji wa maji kwa kila Mtanzania utashuka hadi kufikia mita za ujazo 883 kwa mwaka. Hali hii inatishia usalama na uhakika wa maji ***(water security)*** inayoweza kusabisha migogoro ya kijamii na mdororo wa uzalishaji katika sekta zote.

**Mheshimiwa Spika,** Taarifa mbali mbali za kimataifa juu ya usalama na uhakika wa maji (***Water Security***) zinaoenesha wazi kuwa upungufu wa maji utachangia kwa kiasi kikubwa kuyumbisha Serikali na Tawala mbali mbali duniani. Inaelezewa bayana kuwa matatizo ya maji yanahitaji utatuzi wa haraka ili kuepusha janga la anguko la utawala wa nchi yaani '***State Failure'***

**Mheshimiwa Spika,** Serikali yoyote makini na inayotaka kuimarisha utawala wake ni lazima itambue, izingatie na kuhakikisha upatikanaji wa maji safi na salama kwa wote bila ya ubaguzi; itatue changamato za umasikini ikiwa ni pamoja na umasikini wa maji yaani ***Water Poverty***; misuguano na migogoro ya kijamii itokanayo na masuala ya maji (***Water Conflicts)***, na uharibifu wa mazingira.

**Mheshimiwa Spika,** Kwa hali ilivyo hivi sasa, haieleweki kama Serikali iliyopo madarakani imejipanga vya kutosha kuwahakikishia Watanzania uhakika na usalama wa maji. Zipo dalili nyingi za kukosekana kwa

uhakika na usalama wa maji. Dalili hizo ni pamoja na migogoro kati ya wadau na watumiaji wa maji

**Mheshimiwa Spika,** Methali ya Kiswahili husema 'ni heri kuzuia kuliko kuponya', Kambi ya Upinzani Bungeni inatoa rai kwa Serikali ya Tanzania kwa msisitizo mkubwa sana kwamba ni lazima zerikali iwekeze raslimali fedha na watu katika huduma za Raslimali za Maji. Raslimali za Maji ndicho kitovu cha maji ya kunywa, kuendeshea viwanda, kilimo cha umwagiliaji na shughuli nyingine za kiuchumi na kijamii. Huduma hii ya raslimali za maji ndiyo imekuwa ikiwekewa fedha kidogo zaidi katika bajeti ya Wizara ya Maji na Umwagiliaji.

**Mheshimiwa Spika,** Kwa kutoipa huduma ya Raslimali za Maji umuhimu unaostahili ina maana upungufu wa raslimali za maji utageuka kuwa ni tatizo la kutengenezwa na watu kwa makusudi kabisa yaani ***'man made problem'. Tatizo hili pia limepewa sifa ya kuwa siyo tu ni tatizo la kimfumo, bali ni tatizo la utawala usio bora***. Bajeti finyu kwa huduma ya Raslimali za Maji unaonesha kuwa Serikali inakosa utashi wa kisiasa (lack of political Will) wa kufanya maamuzi sahihi ya uwekezaji katika maendeleo endelevu ya Sekta ya Maji.

### 3.1.2Huduma ya Maji na Usafi wa Mazingira Vijijini

**Mheshimiwa Spika,** Kambi Rasmi ya Upinzani katika Hotuba zake hapa Bungeni imekuwa ikisisitiza na kuitaka Serikali kuanzisha wakala wa maji vijijini, na Serikali ilikubaliana na hoja hiyo.

**Mheshimiwa Spika,** Serikali imekuwa ikitumia fedha nyingi sana zikiwa ni kutoka kwa wahisani kwenye programmu mbalimbali zinazohusu upatikanaji wa huduma za maji vijijini. Kwa bahati mbaya sana fedha hizo zimekuwa zikitumika vibaya kutokana na kutokuwepo kwa usimamizi wa kutosha na mwisho wa siku tatizo la upatikanaji maji linabakia pale pale. Mifano ni mingi hasa ile ya mradi wa visima 10 kwa kila Halmashauri zilivyotumika na tathmini yake bado wananchi hawana maji, kwani visima vilivyochimbwa havitoi maji na hivyo tatizo kubakia pale pale.

**Mheshimiwa Spika,** kwa muktadha huo, naomba kunukuu kile ambacho Kambi Rasmi ya Upinzani ilikisema humu bungeni ;

> *"**Mheshimiwa Spika**, katika Bunge la kumi yaliyotolewa maoni kadhaa ndani ya Bunge lako tukufu kuhusu uanzishwaji wa Wakala ya Maji Vijijini (**Rural Water Agency**) ikiwa na lengo la kuongeza utoaji na usimamiaji wa huduma ya maji kwa wananchi katika maeneo ya Vijijini.*
>
> ***Mheshimiwa Spika**, katika mjadala wa suala hili serikali ilikubali kuundwa kwa Wakala huyu kwa ajili ya huduma ya maji kwa mwaka wa fedha 2015/2016.*
>
> ***Mheshimiwa Spika**, lengo la kuundwa kwa Wakala huyu lilitokana na kuwa na Wakala sawa na Wakala wa Umeme Vijijini. Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inapenda kuhoji hatua zilizofikiwa na serikali katika kuanzisha*

*Wakala huyu kama ambavyo iliahidi hapa Bungeni."*

**Mheshimiwa Spika,** Kambi Rasmi ya Upinzani inataka kufahamu mchakato wa uanzishwaji wa wakala huu wa maji vijijini umefikia wapi?

### 3.1.3Huduma ya Maji, Usafi wa Mazingira na Uondoshaji wa Maji Taka Mijini

**Mheshimiwa Spika,** ni ukweli kwamba miji mingi hapa nchini inapanuka na kuongeza wakazi wake kwa kasi kubwa kutokana na kukua kwa idadi ya watanzania, hivyo huduma ya maji safi na maji taka katika miji ni jambo la muhimu sana katika kuhakikisha afya za wakaazi kwa miji husika.

**Mheshimiwa Spika**, upatikanaji wa maji safi na salama ni changamoto kubwa kwa watu wengi nchini Tanzania. Ingawa kimataifa, Malengo ya Maendeleo ya Milenia (MDG) ya usambazaji wa maji yamefikiwa, upatikanaji wa maji safi nchini Tanzania umezorota. Kwa miongo kadhaa nchi imekuwa nyuma zaidi ya nchi nyingine ambazo ziko kwenye ngazi sawa kimaendeleo na kijiografia.

**Mheshimiwa Spika,** Kwa ujumla, upatikanaji wa maji safi na salama katika miongo miwili iliyopita umepungua kidogo kutoka 55% hadi 53%, na kwa wananchi wa vijijini, imeshuka kutoka 46% hadi 44%. Japokuwa fedha nyingi sana za walipakodi zimeelekezwa uko. Hii ni kwa mujibu wa utafiti wa Twaweza uliotolewa mwezi Aprili 2014, swali la kujiuliza tatizo liko wapi?

**Mheshimiwa Spika,** tafiti za twaweza zinazidi kuonesha kuwa zaidi ya Watanzania watatu kati ya wanne (76%) wanakiri kuwepo kwa changamoto za aina mbalimbali za upatikanaji wa maji. Changamoto kubwa inayotajwa na idadi kubwa ya wakazi mijini na vijijini ni umbali wa kuvifikia vyanzo vya maji. Pia ongezeko kubwa la bajeti ya maji kwa kila Mtanzania kutoka chini Tsh 1,000 hadi zaidi ya Tsh 3,000 katika miaka kumi iliyopita wakati kuna maboresho kwa mujibu wa bajeti zinazopitishwa.

**Mheshimiwa Spika,** kuna changamoto kubwa ya usambazaji maji usio na uhakika kwa watumiaji na hivyo kupelekea gharama kubwa za upatikanaji wa maji. Serikali imekuwa na taarifa nyingi zinazokinzana kuhusu upatikanaji wa uhakika wa maji hasa kwa Mkoa wa Dar es Salaam pamoja na mikoa jirani. Tumeambia kuhusiana na mradi wa uchimbaji wa visima virefu 20 vya Kimbiji na Mpera kama ndio mkombozi au suluhisho la maji kwa mikoa ya Dar es Salaam na Pwani na kwa mujibu wa Mpango wa Kwanza wa Maendeleo ya miaka mitano mradi huu uliwekewa Jumla ya shilingi bilioni 112. Kambi Rasmi ya Upinzani inauliza, je na mpango wa kwanza wa maendeleo ulikuwa ni kiini macho kama ulivyo huu wa pili?

**Mheshimiwa Spika**, Ujenzi wa bwawa la Kidunda ambalo kwa mujibu wa mpango wa kwanza wa maendeleo wa miaka mitano mradi uliwekwa kwenye mpango toka mwaka 2011/12 kwa kuwekewa shilingi 26,800,000,000, na kwa miaka mitano 2015/16 mradi ungetumia jumla ya shilingi bilioni 134 ikiwa shilingi bilioni 112 ni mchango wa Serikali na shilingi bilioni 22

toka kwa wahisani. Lakini kwa maajabu makubwa, sasa hivi Randama inatuonesha kuwa gharama ya ujenzi wa bwawa hilo inatarajiwa kuwa shilingi bilioni 476.2

**Mheshimiwa Spika,** Kambi Rasmi ya Upinzani inasema, Serikali itaendelea kupata hasara na kutotimiza wajibu wake kwa watanzania kama mtindo wa kutokuheshimu utekelezaji wa mipango iliyojiwekea utaendelea. Sasa kupanda kwa gharama za utekelezaji wa mradi wa ujenzi wa bwawa la Kidunda ni muda na kushuka kwa bei ya shilingi yetu.

**Mheshimiwa Spika,** ni muda mwafaka kwa Serikali kuwapa taarifa zenye uhakika wananchi kuhusu upatikanaji wa uhakika wa huduma za maji kwa wakazi wa maeneo ya miradi hiyo.

**Mheshimiwa Spika**, japokuwa takwimu za Serikali zinaonesha kuwa upatikanaji wa maji safi na salama kwa maeneo ya mijini ni asilimia 59 na 26 kwa vijijini, hii ni kwa mujibu wa taarifa ya "demographic and socio economic profile" iliyotolewa na Idara kuu ya Takwimu mwaka 2014.

**Mheshimiwa Spika,** sambamba na hilo, Utafiti wa Sauti za Wananchi-Twaweza, uliotolewa mwezi Mach,2017 umeonesha ya kwamba Upatikanaji wa maji vijijini ulikuwa asilimia 55 mwaka 2014 na asilimia 46 mwaka 2016 – **Ofisi ya Taifa ya takwimu** inaonyesha tofauti ya upatikanaji wa maji kuwa kati ya asilimia 40 na 50 kwa zaidi ya miaka 10 ambapo tafiti tisa kati ya kumi zimeonesha uwiano wa takwimu ndani ya kiwango hiki.

**Wizara ya Maji** nayo imeripoti upatikanaji mkubwa wa maji wa kati ya asilimia 50 na 60 ndani ya kipindi tajwa.Takwimu za **Matokeo Makubwa Sasa** zinaripoti kuongezeka kwa kasi ya upatikanaji wa maji kutoka asilimia 40 mwaka 2013 hadi asilimia 67 mwaka 2015. Kambi Rasmi ya Upinzani inaitaka Serikali ilieleze Bunge hali halisi ilivyo kwa sasa mwaka 2017.

**Mheshimiwa Spika,** mifumo ya uondoaji wa maji taka kwa maeneo mengi ya mijini hasa maeneo ambayo yalikuwa ni mashamba na sasa kutokana na kupanuka kwa miji yamekuwa ni maeneo ya makazi ni tatizo na nijukumu binafsi la mmiliki wa makazi.

**Mheshimiwa Spika,** Hii inatokana na ukweli kwamba wananchi wako mbele zaidi ya taasisi za serikali ambazo ndizo zinatakiwa kupanga miji. Kwa upande mwingine tatizo kubwa ni kuwa miundombinu ya maji taka imezeeka kiasi cha kushindwa kuhimili taka zinazotolewa kutokana na ongezeko kubwa la wakaazi.

**Mheshimiwa Spika,** Kambi Rasmi ya Upinzani inashauri Serikali, kwa maeneo mapya ya makazi waweke mashine za kusafisha maji taka na maji hayo kuingia kwenye mzunguko mpya wa matumizi. Mfano mzuri ni nchi ya Singapore, ambapo maji taka tani milioni 7.5 huzalishwa kwa mwaka na kila mtu anazalisha kilo 1,370 kwa mwaka. Lakini uchafu huo 60% unawekwa kwenye mzunguko na kuwa na matumizi mapya kwa maendeleo ya nchi, ni vyema tukaangalia mbele zaidi katika mipango yetu.

**Mheshimiwa Spika**, katika program hii, Mradi wa Uboreshaji wa Mfumo wa Uondoaji wa Majitaka Jijini Dar es Salaam inaonesha kuwa mikopo toka Serikali ya Korea Kusini na Benki ya Dunia, lakini ukisoma vizuri Randama uk.25 aya ya (iv) mikopo hiyo ni kwa ajili ya kutandika mifumo mipya ya kusafirisha majitaka toka majumbani kwenye maeneo mbalimbali ya Jiji. Lakini Kambi Rasmi inashauri maji taka hayo ya safishwe au "recycled" na yaingie tena kwenye matumizi. Na ndio sababu iliyotufanya kuweka mfano wa Singapore

### 3.1.4. Mradi wa kutoa maji kutoka Ziwa Viktoria hadi katika miji ya Nzega,Igunga, Tabora,Sikonge na Uyui

**Mheshimiwa Spika,** mradi huu unahusisha malengo ya muda mrefu ya kuwapatia huduma ya maji wakazi wapatao milioni 1.1 wa miji tajwa hapo awali pamoja na wananchi vijiji vilivyo kandokando ya bomba kuu la mradi wa Kahama.
Mradi huu umegawanywa katika vipande vitatu vya ujenzi ili kuharakisha kukamilika kwake.

**Mheshimiwa Spika**, mradi mzima utakuwa na kandarasi zenye thamani ya dola za Marekani Milioni 268.35 ambazo ni zaidi ya Shilingi bilioni 600 za Tanzania mjini Tabora kwa mkopo wa benki ya Exim ya nchini India kwa kushirikiana na Serikali ya Tanzani kwa ajili ya ujenzi wa mradi wa maji kutoa Ziwa Victoria na kupeleka katika Manispaa ya Tabora na Halmashauri za Igunga, Uyui, Shinyanga Vijijini na Nzega.

**Mheshimiwa Spika**, Kambi Rasmi ya Upinzani imepokea masikitiko makubwa ya harufu za rushwa katika mchakato wa awali wa kuwapata wakandarasi unaofanywa na watendaji wa Wizara ambao watakuwa ni wasimamizi wakuu wa mradi huu.

**Mheshimiwa Spika,** nyaraka zinaonesha kuwa makampuni yaliyohusika katika zabuni ya ujenzi wa vipande vyote vitatu ni makampuni matano (5),majina tumeyahifadhi kwa usalama wao kibiashara, lakini moja kati ya makampuni hayo kwa ushahidi ilionesha kuwa kulikuwa na mchezo mchafu katika utoaji wa zabuni. Kwani bei ya zabuni kwa makampuni hayo matano zipo lakini vigezo ndivyo havikufuatwa katika utoaji wa zabuni hizo, ***"not always the lowest is the cheapest, what is needed is the competent supervisor" na hawa ma-engineers ambao ni mahiri kusimamia tunao na wanalipwa vyema.***
Mlalamikaji alitoa ushahidi wake kwa Mheshimiwa Waziri na hakuna hatua zilizochukuliwa. Hii ni kasoro kubwa sana kwani, jambo hili linatupa wasiwasi hata ukamilikaji wa mradi huu.
Kambi Rasmi ya Upinzani inamtaka Mhe.Waziri aliangalie kwa kina suala hili, kwani linamtia doa hata yeye ambaye ndiye msimamizi mkuu wa wizara hii. Kwani miongoni mwa malalamiko yaliyotajwa ni Afisa mmoja Wizarani kufoji email na kutunga uongo uliotumika kufanya maamuzi ya nani apewe zabuni na nani asipewe.

**Mradi wa Maji Lindi Mjini**

**Mheshimiwa Spika,** Mradi wa Maji Lindi Mjini eneo la Ng'apa unajengwa na kampuni ya Overseas Infrastructure Alliance Private Limited ya India, mkandarasi huyo alianza kazi baada ya mradi kuzinduliwa rasmi na Mhe Rais Mstaafu Jakaya Kikwete Agosti 8,2015. Mradi huo unatekelezwa kwa mkopo kutoka Benki ya Maendeleo ya Ujerumani (KFW) na Umoja wa Ulaya (EU)

**Mheshimiwa Spika,** Mheshimiwa Spika, tukumbuke kuwa Mhe WAZIRI Mkuu, Kassim Majaliwa, mwezi Oktoba mwaka 2016 alimsimamisha kazi Mkurugenzi wa Mamlaka ya Maji Lindi (LUWASA), Mhandisi Adam Alexander kwa matumizi mabaya ya ofisi pamoja na kushindwa kusimamia ujenzi wa kituo cha kuzalisha maji katika manispaa hiyo (Mradi wa Ng'apa).

**Mheshimiwa Spika**, Mheshimiwa Rais katika ziara yake mkoani Lindi alimtaka mkandarasi huyo kuhakikisha kuwa inakamilisha ujenzi wa Mradi wa Maji wa Ng'apa uliopo mkoani Lindi unakamilika ndani ya miezi minne na si vinginevyo huo na sio kuleta visingizio**.**

**Mheshimiwa Spika**, Mheshimiwa Waziri alisema kuwa hadi sasa mradi huo umefikia asilimia 85 na kwamba mkandarasi amesimamisha kazi kutokana na kuishiwa fedha. Kambi Rasmi ya Upinzani inataarifa kuwa fedha za ujenzi wa mradi huo zimewekwa kwenye Akaunti Mkandarasi iliyopo nchini India, na hivyo fedha hizo

kukosa uangalizi wa msimamizi wa Mradi huo (Consultant).

### 3.2 Huduma za Umwagiliaji- Tume ya Taifa ya Umwagiliaji-(Fungu 05)

**Mheshimiwa Spika,** kilimo cha umwagiliaji katika nchi hii kimekasimiwa chini ya mamlaka ya Tume ya Taifa ya Umwagiliaji (fungu 05), takwimu zinatuonesha kuwa kwa nchi yetu ina jumla la hekta milioni 29.4 zinazofaa kwa umwagiliaji, na hekta milioni 2.3 zina uwezekano mkubwa wa kumwagiliwa, hekta milioni 4.8 zinauwezekano wa kati na hekta million 22.3 zina uwezekano mdogo wa kumwagiliwa.

**Mheshimiwa Spika,** kwa mujibu wa taarifa ya utekelezaji inaonesha kuwa ifikapo 2021 eneo lenye ukubwa wa hekta milioni 1 liwe limeendelezwa kwa kilimo cha umwagiliaji, lakini kwa sasa ni eneo la hekta 468,338 ndilo linamwagiliwa.

**Mheshimiwa Spika,** Kambi Rasmi ya Upinzani inawasiwasi kuwa, lengo la kufikia umwagiliaji wa hekta milioni 1, wakati tunakwenda kwenye uchumi wa viwanda na kilimo ndio injini ya kutoa malighafi nyingi itakayohitajika katika viwanda. Ni dhahiri kwamba uwezekano mkubwa wa maandiko hayo yatabakia kwenye makabrasha tu na sio kwa utekelezaji.

**Mheshimiwa Spika,** Sekta ya huduma za umwagiliaji maji (kifungu 05) iliombewa bajeti ya Tshs 39,876,141,428 ambapo kati ya hizo, Tshs 35,369,529,428

ni kwa ajili ya maendeleo na Tshs 4,206,827, 000 ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida. Bajeti hii ni pungufu ya ile ya mwaka uliopita kwa asilimia 26.

**Mheshimiwa Spika,** Mwenendo wa miezi tisa yaani kati ya Julai 2016 na Machi 2017, ni wa kustua na kusikistisha, hususan ukilinganisha umuhimu wa Sekta ya Umwagiliaji katika muktadha wa mapinduzi ya viwanda yanatarajiwa kutokea nchini Tanzania.

**Mheshimiwa Spika,** Tanzania ni nchi ya kilimo, na uchumi wa viwanda utabebwa kwa kiasi kikubwa na kilimo. Ili kufikia azma ya uchumi wa viwanda, mikakati iliyopo katika Sekta ya Kilimo hususan kilimo cha umwagiliaji, ni kupanua eneo la uzalishaji kwa takriban hekta millioni 1.5 ili kuongeza uzalishaji kwa asilimia 25 na kunufaisha zaidi ya kaya 2.3 milioni au watu wapatao milioni 12.

**Mheshimiwa Spika,** Ndoto hii ya kukuza uzalishaji haitakamilika iwapo fedha zilizoidhinishwa na Bunge hazitatolewa ili kufanikisha malengo yaliyokusudiwa.

**Mheshimiwa Spika,** Kuna matatizo mengi ya matumizi ya fedha zinazotolewa na Serikali kwa ajili ya miradi ya umwagiliaji hapa nchini, Naibu waziri ofisi ya rais, Tamisemi, Mh.Seleman Jaffo katika ziara yake katika jimbo la Mwanga alisikitishwa na utekelezaji wa mradi wa maji ya umwagaliiji katika kijiji cha Kivulini wilaya ya Mwanga kujengwa chini ya kiwango huku halmashauri ikishindwa kujua thamani  halisi ya mashine zilizofungwa katika mradi huo ambao unatarajia kugharimu zaidi ya shilingi bilioni 1.6

Mheshimiwa Spika, Mradi wa umwagiliaji wa Kiwalala katika bonde la Lukuredi halmashauri ya wialaya ya Lindi, umegharimu zaidi ya shilingi milioni 600 lakini hadi sasa mradi haufanyikazi. Na maelezo yanayotolewa ni kwamba Mkandarasi alikosea wakati amafanya usanifu, hivyo kwa eneo uliopo haliwezi kutoa tija na hivyo mradi ndio umekufa kifo cha mende kama miradi mingine mingi kama vile Kinyope mradi wa hekta 400 katika Jimbo la Mchinga.

**Mheshimiwa Spika,** Katika hali kama hii ni halmashauri ngapi zinapoteza fedha za walipa kodi wan chi hii kwa kushindwa kusimamia fedha za miradi?

**Mheshimiwa Spika,** Katika mwaka wa fedha 2016/2017 vitengo/Idara nne kati ya saba hazikupatiwa fedha kabisa kwa ajili ya kuendesha shughuli zake. Idara/Vitengo hivyo ni Uhakiki na Udhibiti wa Ubora, Huduma za Uedeshaji na Uwezeshaji wa Umwagiliaji, Utafiti na Uhamasishaji wa Teknolojia za Umwagiliaji na Mazingira na Jamii.

**Mheshimiwa Spika,** Ni jambo la kushangaza na fedheha kuona kwamba pamoja na Serikali iliyopo madarakani kusistiza uchapaji kazi wa hali ya juu, sekta muhimu kama hii ya umwagiliaji ambayo inategemewa katika kuinua productivity ya kilimo iliyodorora katika miaka ya karibuni, inanyimwa fedha za kuweka miundombinu inayohitajika kwa kazi hiyo. Itakuwaje kutekeleza ***"Kauli mbiu ya Hapa Kazi Tu"*** kama vitendea kazi havipatikani?

**Mheshimiwa Spika,** Uzoefu unaonesha bila ya kuwa na uhakika na usalama wa maji, azma ya kupanua kilimo

na kukifanya kiwe cha kisasa, endelevu na hatimaye kupata mapinduzi ya viwanda itabakia kuwa ni nadharia kwenye makabrasha tu bila ya kuwa na utekelezaji wowote.

**Mheshimiwa Spika,** kutokana na ukweli kwamba, tunakokwenda tutakuwa na upungufu mkubwa wa maji kwa ajili ya matumizi ya kibinadamu, kutokana na mabadiliko ya Tabianchi. Hivyo katika kutekeleza jukumu hilo la umwagiliaji ni lazima Tume ya umwagiliaji ichague aina ya umwagiliaji ambayo itatumia maji kidogo wakati huo kuzalisha kwa tija. Aidha, Kambi Rasmi ya Upinzani inaamini kabisa kuwa kufanya ufuatiliaji wa miradi ambayo ilikwisha pata fedha za utekelezaji na kuona ni kwa vipi miradi hiyo ya umwagiliaji inawanufaisha wananchi katika maeneo husika.

**Mheshimiwa Spika,** District Agriculture Sector Investment Project (DASIP) ni Mradi uliokuwa wa miaka saba (7) ulianza mwaka 2006 hadi 2013 na mradi ulihusisha wilaya 28 za mikoa ya Kagera, Kigoma, Mara, Mwanza na Shinyanga ambao ulikuwa ni mkopo wa (***Unit of Account)*** UA million 58.01 kutoka Benki ya Maendeleo ya Africa (ADB). Mradi ulitekelezwa kupitia mfumo wa ASDP katika utaratibu wake wa utekelezaji wa miradi chini ya Project Coordination Unit (PCU).

***NB:*** *UA moja ni sawa na 1.567 US$ kwa mwaka 2009 kwa thamani ya mwaka huo.*

**Mheshimiwa Spika,** Mradi ulikuwa na lengo la kuongeza tija na mapato kwa jamii ambazo ni wanufaikaji wa mradi na progamu nzima ya DASIP. Mradi huu ulihusisha skimu za umwagiliaji 23 zilizokuwa na thamani ya shilingi 16,600,251,799.40 (AfDB funds) na fedha zilizolipwa kwa skimu hizo 23 lakini hadi sasa hakuna hata skimu moja iliyokamilika kwa asilimia 100 ilikuwa ni shilingi 9,209,934,228.16 (AfDB & DIDF). Zifuatazo ni baadhi tu ya Skimu hizo kati ya zile 23; Pia Jumla ya shilingi 1,521,699,500.00 zilikuwa zimetengwa kwa ajili ya utaalam ushauri (consultancy) na kiasi cha shilingi 1,408,742,558.00, kililipwa kwa wataalam washauri wa miradi hiyo. Hapa ni baadhi ya skimu zilizokuwemo ndani ya Programu hiyo na thamani ya kila skimu na fedha zilizolipwa kwa mkandarasi;

i. Kahanga iliyopo Kahama ya thamani ya shilingi 774,164,345 na mradi ulisainiwa tarehe 20.03.2013 na ulitakiwa kuchukua siku 210, hadi mkandarasi anaondoka alilipwa shilingi 273,149,775. Lakini mradi hadi sasa haufanyikazi.
ii. Kinamwigulu skimu-Maswa, mradi ulikuwa na thamani ya shilingi 698,189,988. Na mkataba wa ujenzi ulisainiwa 01.02.2013 na ulitakiwa kukamilika 07.08.2013, mkandarasi alilipwa shilingi 628,361,988.3 mradi hadi sasa haufanyikazi kwa ukamilifu wake.
iii. Kisangwa Skimu-Bunda, thamani ya mradi ilikuwa ni shilingi 385,901,500. Mkataba ulisainiwa 07.05.2012 na ulikuwa wa siku 150 kukamilisha mradi. Mkandarasi alilipwa shilingi 259,653,118. Mradi haufanyikazi
iv. Kyakakera Skimu –Misenyi mradi uliokuwa na thamani ya shilingi 497,120,784 na ulisainiwa

20.3.2013 na ulitakiwa kukamilika ndani ya siku 150. Serikali ilimlipa Mkandarasi jumla ya shilingi 429,268,874.4 wakati kazi kwa mujibu wa mkataba ilikuwa imekamilika kwa asilimia 31 tu.

v. Lutubiga Skimu –Busega, mradi ulikuwa na thamani ya shilingi 799,047,665. Ulisainiwa 5.2.2013 na kazi ilitakiwa kukamilika ndani ya siku 240. Lakini hadi mkandarasi anaondoka site kazi ilikamilika kwa asilimia 49 tu.

vi. Lwenge Skimu-Geita, mradi ulikuwa na thamani ya shilingi 434,637,358. Na ulitakiwa kukamilika ndani ya siku 150 baada ya kusini mkataba hapo tarehe 01.02.2013. Lakini hadi Mkandarasi anaondoka site kwa kukamilisha asilimia 59 tu ya kazi na alilipwa shilingi 391,125,000.

vii. Masinono Skimu- Musoma, mradi ulikuwa na thamani ya shilingi 1,248,038,427.67 na mkataba ulifungwa 09.05.2013 na kazi ilitakiwa kukamilika kwa muda wa siku 270. Serikali ililipa jumla ya shilingi 265,681,080. Hadi sasa mradi haufanyikazi.

viii. Mgondogondo Skimu-Kibondo, mradi ulikuwa na thamani ya shilingi 330,453,742. Mradi ulitakiwa kukamilika ndani ya siku 180 tu, lakini hadi mkandarasi anaondoka site alikwishalipwa jumla ya shilingi 297,407,107.8 wakati kazi ilikamilika kwa asilimia 53 tu.

ix. Mwagila Skimu-Meatu, uliokuwa na thamani ya shilingi 1,165,132,300. Na ulisainiwa 05/02/2013 mradi ulitakiwa kukamilika ndani ya siku 180, lakini Serikali ililipa shilingi 1,164,006,962. Lakini hadi sasa mradi haufanyikazi.

x. Mwasubuya Skimu-Bariadi, mradi ulikuwa na thamani ya shilingi 1,204,646,601. Ulisainiwa tarehe 20.03.2013 na ulitakiwa ukamilike ndani ya siku 270. Serikali ilimlipa mkandarasi shilingi 215,884,150.71. lakini mradi huo hadi leo haufanyikazi.

**Mheshimiwa Spika,** Kambi Rasmi ya Upinzani inamtaka Mheshimiwa Waziri alieleze Bunge wahusika wa upotevu wa / hasara ya fedha kama zilivyowekwa hapo awali ni hatua gani zimechukuliwa kwani hadi sasa miradi hiyo ya skimu za umwagiliaji haifanyikazi na fedha hizo zilikuwa ni mkopo toka Benki ya Maendeleo ya Afrika.Wataalam washauri wa miradi hiyo ambao walikuwa ndio wasimamizi wakubwa wa miradi hiyo ni hatua gani zimechukuliwa dhidi yao?

**Mheshimiwa Spika,** Mpaka hivi sasa kilimo cha umwagiliaji kinatumia kiwango kikubwa cha maji kuliko sekta nyingine yoyote, lakini ni kiwango kidogo sana cha maji kinatumika kwa tija.

**Mheshimiwa Spika,** Taarifa ya Wizara ya Kilimo na Uhakika wa Chakula zinaonesha kuwa ni asilimia 15 tu ya maji yanayochukuliwa kutoka katika vyanzo mbali mbali vya maji ndiyo inayotumika vizuri (Wizara ya Kilimo na Uhakika wa Chakula, ACRP 2014). Miundombinu ya umwagiliaji ni chakavu na ile mipya ina makosa mengi ya kiufundi (ASDP II).

**Mheshimiwa Spika,** Kilimo cha umwagiliaji vilevile kimegubikwa na migogoro kati ya watumiaji wa maji, na kimesababisha nadhara makubwa. Kati ya watumiaji wa raslimali za maji. Tumeona madhara

makubwa ya mapigano kati ya wakulima na wafugaji wakigombea maeneo yenye maji kwa ajili ya kilimo na mifugo.

**Mheshimiwa Spika**, *"Integrated Water Resource Management (IWRM) Integrated Water Resources Management (IWRM) is a comprehensive approach to water resource management that views water as a single resource with competing uses and inter linkages with the ecological, social and economic systems. Through IWRM, water is treated as an economic, social, and environmental good; and IWRM helps ensure that policies and options that guide water resources management are analyzed within an integrated framework"*

**Mheshimiwa Spika,**Kambi Rasmi ya Upinzani inaitaka Serikali iwaeleze wananchi ni kwa vipi Wizara hii ya Maji na Umwagiliaji inapambana na mabadiliko ya Tabianchi jambo ambalo ni kisababishi kikubwa cha upungufu mkubwa wa maji kwa makundi mbalimbali ya watumiaji, hasa katika kuchagua na kuhamasisha aina ya kilimo cha umwagiliaji kinachotumia maji kidogo na kutoa tija kubwa?

## 4.0: Mapitio ya Maombi ya Fedha 2017/2018

**Mheshimiwa Spika**, kwa kuangalia takwimu za maombi ya fedha za maendeleo kwa wizara (fungu 49) zinaonesha kuwa kwa mwaka wa fedha 2015/16 ilipewa shilingi 141,244,873,622 kati ya hizo fedha za ndani ziliwa shilingi 100,394,810,359 na za nje zikiwa shilingi 40,860,063,263. Mwaka 2016/17 ilitengewa jumla ya shilingi 915,193,937,771 kati ya hizo za ndani zikiwa ni shilingi 690,155,000,000 na za nje zikiwa shilingi 225,038,937,771.

**Mheshimiwa Spika**, kwa mwaka wa fedha 2017/18, Wizara inaomba kupatiwa jumla ya shilingi 632,606,748,000 kati ya hizo shilingi 408,617,643,000 ni fedha za ndani na shilingi 214,989,105,000 zikiwa ni fedha za nje.

**Mheshimiwa Spika,** takwimu zinaonesha kuwa fedha za ndani kwa wizara kwa kulinganisha mwaka jana na mwaka huu kuna tofauti ya shilingi 281,537,357,000. Kambi Rasmi inataka kufahamu kama Serikali inavyodai kila mara kuwa makusanyo ya mapato ya ndani yanaongezeka kila mwaka inakuwaje inapunguza mgawo wa fedha za maendeleo kwa sekta muhimu kama maji, ambayo inawagusa watanzania wote na pia ndiyo injini ya kuifanya Tanzania kuwa nchi ya uchumi wa Kati?

## 5.0 Hitimisho

**Mheshimiwa Spika**, ni ukweli kuwa, Serikali pamoja na wadau wa maendeleo, taasisi zisizo za kiserikali pamoja na taasisi za kidini kwa muda tofauti zimeweka fedha zao kwenye miradi kadhaa inayodhamiria kuhakikisha upatikanaji wa maji safi na salama kwa wananchi wetu, Kambi Rasmi ya Upinzani inaliona jambo hili sio suala la kujadili kwani liko wazi.

**Mheshimiwa Spika**, ni miradi mingi sana ambayo imetumiwa fedha nyingi sana za walipa kodi wa nchi hii, hasa miradi ya vijiji 10 kwa kila wilaya, ambapo Serikali ilishindwa kusimamia miradi hiyo na sasa hivi takwimu zinaonesha kuwa miradi imekamilika wakati huohuo wananchi wengi katika vijiji husika hawana maji.

**Mheshimiwa Spika**, sio hilo tu, skimu nyingi za umwagiliaji katika nchi yetu, fedha za mikopo au halmashauri au fedha za misaada toka kwa wadau wa maendeleo zimezama na miradi imekuwa kama magofu hakuna uzalishaji unaofanyika.

**Mheshimiwa Spika,** Kambi Rasmi ya Upinzani inataka kuishauri Serikali kwamba miradi itakpokuwa inafaanza ni vyema wananchi wakapewa taarifa kuhusu thamani halisi ya mradi na unatakiwa kumalizika lini ili nao kwa nafasi zao wawe ni wasimamizi vivuli wa raslimali za Serikali. Mfano ni mradi wa maji wa Kahama Tabora na wilaya zake, randama haioneshi ni mradi wa shilingi ngapi kwa kila hatua japokuwa zabuni tayari zimefunguliwa na wakandarasi tayari wamepewa kazi na hivyo waheshimiwa wabunge wasaidie katika ufuatiliaji.

Kambi Rasmi ya Upinzani inasema, ni muda mwafaka sasa wananchi kushirikishwa katika shughuli za maendeleo yanayowahusu kwani wao ndio watakuwa wasimamizi wakubwa wa miradi husika, badala ya tabia iliyopo sasa ya wao kuona watu wanafanyakazi nao kuwa watazamaji tu.

**Mheshimiwa Spika,** baada ya kusema hayo kwa niaba ya Kambi Rasmi ya Upinzani, naomba kuwasilisha.

**………………………**

**Hamidu Hassan Bobali (Mb)**
**Waziri Kivuli na Msemaji Mkuu wa Kambi Rasmi ya Upinzani-Wizara ya Maji na Umwagiliaji**
**10/05/2017**